Shuguli za Kiswahili - Grade 4 Term 1 Exams 2023

MASWALI

1. **Soma kwa sauti (alama 10)**
   Mazingira safi ni muhimu kwa afya ya kila kiumbe. Maradhi mengi hutokana na uchafu katika mazingira tunamoishi. Ugonjwa wa Malaria husababishwa na uchafu katika mazingira. Mbu wanaoambukiza malaria huishi kwenye mikebe yenye maji iliyotupwa ovyoovyo.
   Tunapaswa kuyalinda ili yawe safi. Na pia tulale ndani ya chandarua kilichotibiwa.
2. **KUONGEANA KUSIKILIZA**
   <u>Tamka maneno yenye silabi tatanishi (alama 5)</u>
   piga
   pika
   tamu
   damu
   jaja
   chacha
   bata
   pata
   chalijali
3. **<u>Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo</u>**
   Mwalimu wetu alituambia kwamba ni vyema mtoto awe na nidhamu.
   Alisema huwa si vyema mtoto. kuwa, mkatili, mlafi na mchokozi. Mtoto mwenye tabia hizi mbaya huchukiwa na watu wote kijijini. Siku moja jirani yetu alitutembelea nyumbani kwetu. Jina lake aliitwa Furaha. Furaha alipenda kucheza sana na kubeba vitu chumbani badala ya kuomba mama yake ruhusa kabla ya kubeba.
   Ilipofika jioni Furaha aliambia mama kuwa anahisi njaa na angetaka ale chakula au anywe uji.. Mama yake alimwambia asubiri ampikie uji. Baada ya muda mfupi Furaha hakusubiri awekewe uji kwa kikombe. Alisimama na akajiwekea uji moto. Alijaribu kuunywa akashindwa. Kwa bahati mbaya uji moto ulimumwagikia nguoni. Alikimbia mbio huku akilia kwa uchungu mwingi.
   a. Taja mambo matatu ambayo mtoto hapaswi kuwa nayo .....
   b. Mwalimu aliwafunza wanafunzi ni vyema kuwa na? ..... .
   c. Nani aliyempikia furaha uji? .....
   d. Mtoto mwenye tabia mbaya ..... na watu wote.
   e. Nani aliyependa kucheza? .....
   f. Nani hakuomba ruhusa? .....
4. Jaza pengo
   a. Rafiki yako darasani anaitwaje?
      .....